THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL

CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION EXAMINATION

NOVEMBER 1998

021

# KISWAHILI

(Kwa Watahiniwa walioko Shuleni na wa Kujitegemea)

MUDA: Saa 3

---

## MAAGIZO

1. Jibu maswali MANANE (8) tu, maswali MANNE (4) kutoka Sehemu A, na maswali YOTE ya Sehemu B.
2. Zingatia maagizo ya kila sehemu na ya kila swali.

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

Scanned with CamScanner

## SEHEMU A: FASIHI

### Kifungu (i) Fasihi Simulizi

1. Kwa kutoa mifano isiyopungua mitano, eleza jinsi matumizi ya viungo vya mwili vinavyokamilisha Fasihi Simulizi.

AU

2. Chagua tamathali za semi tano (5) na kuzielezea jinsi zinavyosaidia kueleweka kwa dhamira za tanzu za Fasihi Simulizi.

## FASIHI ANDISHI

### Kifungu (ii) Ushairi

| | | |
|---|---|---|
| Malenga Wapya | - TAKILUKI | - (DUP) |
| Diwani ya Mloka | - C. Mloka | - (B.P.) |
| Diwani ya Ustadh | - A. Andanenga | - (B.P.). |

3. Miongoni mwa kazi za msanii ni kuweka wazi maovu yaliyojificha na kuyakemea. Chagua washairi wawili kati ya waliotajwa hapo juu na jadili jinsi wanavyotekeleza wajibu huo.

AU

4. Kwa kutumia washairi wawili kati ya washairi waliotajwa hapo juu, jadili jinsi wanavyofanana na kutofautiana katika miundo ya ushairi wao.

### Kifungu (iii) Riwaya/Hadithi

| | | |
|---|---|---|
| Kusadikika | - S. Robert | (Nelson) |
| Hiba ya Wivu | - Z. Mwanga | - (R.P.) |
| Zawadi ya Ushindi | - B. Mtobwa | - (TPH) |

5. "Migogoro baina ya haki na dhuluma ni suala linalojitokeza katika kazi nyingi za fasihi". Chagua riwaya mbili kati ya hizo zilizotajwa hapo juu na ujadili kauli hii.

AU

6. Chagua wahusika wawili mmoja kutoka kila riwaya kati ya hizo zilizotajwa hapo juu na eleza jinsi wanavyodhihirika kuwa mfano wa wapigania haki za wanyonge.

### Kifungu (iv) Tamthiliya

| | | |
|---|---|---|
| Ngoswe - Penzi Kitovu cha Uzembe | - E. Semzaba | (ESC) |
| Mfalme Juha | - F. Topan | (DUP) |
| Hawala ya Fedha | - A. Lihamba | (TPH). |

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

Scanned with CamScanner

7. Kwa kutumia tamthiliya mbili kati ya hizo hapo juu onesha ukweli kwamba bidii bila maarifa ni kazi bure.

AU

8. "Tamthiliya hizi zinaonesha suala la utapeli la wahusika wao". Kwa kutumia tamthiliya mbili kati ya hizo hapo juu fafanua utapeli unaofanywa na wahusika hao.

## SEHEMU B: LUGHA

9. UFAHAMU:

Soma kifungu cha habari kifuatacho kisha jibu maswali.

Mpango wa kilimo cha pamba ulileta maafa mengi. Ardhi iliyochaguliwa ilikuwa haifai hivyo ilitoa mavuno haba. Mpango wa kazi uliendeshwa kikatili. Kwa jumla hapakupatikana faida yoyote. Wafanyakazi wa Kizaramo walikataa malipo ya senti 35 waliyopewa kwa kazi yao ya mwaka wa kwanza.

Mwezi Julai 1905, wafanyakazi hao waliamua kuanzisha mapigano. Usiku wa Julai 31, Wamatumbi walimfukuza akida wao waliomchukia, pamoja na wageni wengine wote kutoka vilimani mwao. Vita vya Maji Maji vilianza. Kwanza vilienea katika sehemu yote ya kilimo cha pamba, sehemu za kati na chini ya Mto Rufiji, halafu vikaenea Uluguru, Uwanda wa Mahenge, mabonde ya Lukuledi na Kilombero. Tarehe 30 Agosti, watu elfu nane wa makabila ya Wambunga na Wapogoro wakiwa wamejihami na mikuki, walijaribu kuihujumu ngome ya Mahenge na kuiteka nyara mizinga ya Wadachi kwa mikono yao mitupu. Lakini walishindwa na wengi wao walianguka katika jaribio hilo.

Mapema Septemba mwaka huo, Wangoni walijiunga katika vita hivyo, lakini pia nguvu zao za mapigano zilivunjwa. Ilipofikia mwezi Novemba, Wadachi walikuwa walikwisha jiimarisha Kusini Nyanda za Juu. Wananchi walikuwa wamegawanywa. Huko Magharibi Wadachi walikuwa wamefaulu kuzingira na kuvunja kabisa nguvu za viongozi wa Wangoni na Wabena. Mashariki, Wangindo wakiwa na wananchi wengine, walipigana kwa muda mrefu vita vya msituni hadi Januari 1907 ambapo kiongozi wao, Abdallah Mapanda aliyekuwa msasi wa ndovu aliuliwa kwa risasi.

Halafu pakaingia njaa kuu. Patakosaje kutokea zahama hiyo iwapo nyumba na mashamba yalichomwa moto? Katika vita na njaa takriban wananchi elfu sabini na tano walipoteza maisha.

Vita vya Maji Maji vilikuwa maarufu kwa sababu tatu: Kwanza, vita hivi vilikuwa jaribio la kutafuta njia mpya ya kujipatia uhuru, ingawa umoja halisi wa wananchi haukupatikana. Pili vita hivi vilijaribu kuwaunganisha wananchi bila kujali makabila yao. Dini ilitumiwa kuleta umoja huu. Kila mpiganaji 'aliyanywa maji ya dawa' kwa kunyunyiziwa mwilini mwake. Baada ya hapo iliaminika risasi haitampenya; wakati huo huo askari huyo ameimarishwa kiudugu katika vita. Mwanzo, maji hayo yalitolewa na mzimu wa Kolelo, katika milima ya Uluguru. Baadaye maji yalihusishwa na imani ya majilio ya ulimwengu mpya; usiokuwa na maovu. Nguvu ya Wadachi ilipokithiri, umoja huu wa Maji Maji ulivunjika, ukawa vikundi vikundi vya kikabila.

Labda jambo la tatu ndilo muhimu zaidi. Baada ya vita vya Maji Maji, wananchi walitafuta njia mbalimbali za kujipatia uhuru - na ukapatikana.

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

Scanned with CamScanner

MASWALI:

(i) Toa sababu mbili zilizofanya mpango wa kilimo cha pamba usifanikiwe.

(ii) Kwa nini unafikiri Wamatumbi walimfukuza akida wao?

(iii) Taja mikoa mitano iliyoshiriki vita vya Maji Maji kwa mujibu wa makala haya.

(iv) Mkoa upi ulikuwa wa kwanza na wa mwisho kupigana vita vya Maji Maji?

(v) Wajerumani walitumia mbinu gani za kuwashinda wazalendo?

(vi) Taja hoja mbili kuu zinazofanya vita vya Maji Maji viwe maarufu hapa nchini.

(vii) Kwa nini viliitwa vita vya "Maji Maji"?

(viii) Dini ipi iliyohusika katika vita vya Maji Maji?

(ix) Toa ushahidi kutoka makala haya kuwa 'Maji' hayakufaulu kama kinga dhidi ya risasi.

(x) Licha ya wazalendo kushindwa, vita vya Maji Maji vimefaulu jambo lipi?

10. Andika insha isiyopungua maneno 250 juu ya mada moja kati ya hizi zifuatazo:

(a) Video katika vyombo vya usafiri.

(b) Umuhimu wa kumuelimisha msichana.

(c) Athari za ulevi.

(d) Penye ukweli uongo hujitenga.

11. Changanua sentensi zifuatazo kwa njia ya matawi.

(a) Baba na mama tuwaheshimu sana.

(b) Wanafunzi wanasoma sana ila wanachokisoma hawakizingatii.

12. Jadili matumizi matano (5) ya Kiunganishi "kwa". Kwa kila utumizi toa mfano mmoja.

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

Scanned with CamScanner